

**TAARIFA FUPI YA KIKUNDI CHA WANAWAKE – KIMBOLEMBOLE VICOBA  
KILICHOPO NYAMWAGE, KATA YA MBWARA WILAYA YA RUFJI KWA  
KIONGOZI WA MBIO ZA MWENGE WA UHURU 2017.**

Ndugu Kiongozi wa mbio za Mwenge Kitaifa ndugu Amour Hamad Amour; sisi akina mama wa Nyamwage tunakukaribisha kwenye kikundi chetu cha kuweka na kukopa (VICOBA). Aidha, tunakupongeza kwa jukumu kubwa la Kitaifa ulilonalo.

Ndugu kiongozi wa mbio za Mwenge, Kikundi chetu kina jumla ya wanachama 13 ambao ni kinamama tuliojiunga na kuunganisha nguvu zetu kwa pamoja ili tuweze kukusanya mtaji kwa lengo la kujiongezea kipato na kujajiri.

Kikundi chetu kinajishughulisha na VICOBA, ufugaji kuku wa kienyeji na kilimo cha bustani na matunda.

Ndugu kiongozi wa mbio za Mwenge, tunapenda kuishukuru Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji kwa ushirikiano wanaotupatia ikiwa ni ushauri pamoja na uwezeshaji kupitia Mfuko wa maendeleo ya wanawake (WDF) ambapo kwa mwaka 2015/2016 tumefanikiwa kupata mkopo wa Tsh 2,000,000.00 (milioni mbili tu) ambayo ilituwezesha kuongeza mtaji wetu na tumelipa zote lakini tumeahidiwa kukopeshwa tena mwaka huu na Halmashauri yetu.

Kwa sasa kikundi chetu kina Jumla ya Tsh 6,000,000.00 (milioni sita tu) ambazo zipo kwenye akaunti yetu ya Benki Na. 21310003257 Kimbolebole NMB Kibiti na fedha zingine tunatunzia kwenye sanduku letu la VICOBA tulilonalo hapa kijijini kwetu.

Ndugu Kiongozi wa mbio za Mwenge, kwa heshima na taadhima tunakuomba utukagulie mradi wetu wa VICOBA.

Ni sisi kinamama wa Kimbolebole VICOBA Nyamwage.

*“Mwenge Oyee”*

**SALOME PASTORY MSURA**

**KATIBU WA KIKUNDI CHA KIMBOLEMBOLE**